# CREATING HOPE IN CONFLICT:

## A HUMANITARIAN GRAND CHALLENGE

MAOMBI YA MAPENDEKEZO YA UFADHILI

29 Juni, 2023

USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE
UKaid from the British people
Ministry of Foreign Affairs of the Netherlands
WITH SUPPORT FROM Grand Challenges Canada® Grands Défis Canada

# MUHTASARI MKUU

Leo, zaidi ya watu milioni 339 wanahitaji msaada wa kibinadamu huku rasilimali zinazohitajika kushughulikia mahitaji haya zikidorora.[1] Mamilioni ya watu walio hatarini zaidi katika maeneo yenye mizozo kwa sasa hawafikiwi na utoaji wa misaada ya kibinadamu. Kadiri urefu na ugumu wa mizozo ya silaha inavyoongezeka, inakuwa vigumu zaidi kuwafikia watu walioathirika katika maeneo yasiyo salama ili kupata msaada muhimu wa kibinadamu na kuboresha maisha yao.

Tangu mwaka wa 2018, Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani, Ofisi ya Mambo ya Nje ya Uingereza, Jumuiya ya Madola na Ofisi ya Maendeleo, Wizara ya Mambo ya Nje ya Uholanzi, Idara Masuala ya Kimataifa Nchini Canada, na Grand Challenges Canada zimeshirikiana katika *Kuleta Matumaini katika Mizozo: Ushirikiano katika Usaidizi wa Kibinadamu (CHIC).* Muungano huu uliungana ili kufadhili na kuharakisha suluhisho za kuboresha usaidizi wa kibinadamu kwa watu walioathiriwa na mizozo. Mpango huu unaunga mkono suluhisho zinazolenga kukidhi vyema mahitaji ya jamii zilizoathiriwa na mizozo, na suluhisho ambazo zina uwezo wa kushawishi mabadiliko ya kiwango cha mifumo katika sekta ya usaidizi wa kibinadamu.

Kupitia Ombi hili la Kuomba ufadhili, tutatoa ufadhili wa kwanza kufikia hadi miradi 20 wa **CAD $250,000** kila moja, pamoja na usaidizi wa jumla wa kuongeza kasi, katika kipindi kisichozidi miezi ishirini na nne (24) kuanzia Aprili 2024.

Tunatafuta hasa, uvumbuzi unaokusudiwa jamii zilizoathiriwa na mizozo ambao unashughulikia changamoto au kutafuta kuboresha utoaji wa huduma katika maeneo yafuatayo:

- Ufikiaji wa Nishati
- Ufikiaji wa habari muhimu za kuokoa maisha
- Ufikiaji wa Bidhaa na Huduma za Afya

Maombi lazima yaonyeshe mchango wenye maana kutoka kwa jamii zilizoathiriwa ambazo watuma maombi wanalenga kuhudumia, na upendeleo utapewa suluhisho zinazomilikiwa na wahudumu wa kibinadamu mashinani wanaotoka katika jamii zilizoathiriwa na mizozo wanayolenga kuhudumia.

Timu za miradi itakayofanikiwa zitajumuisha watu wanaoelewa muktadha wa kipekee wa majanga yanayotokana na mizozo, na wale wanaoweza kuonyesha uwezo wa kuunda, kujaribu, kuboresha na kubadili ili kupanua uvumbuzi kwa ajili ya kuleta mabadiliko kwa watu walioathiriwa na mizozo.

Kufikia mwisho wa kipindi cha kutolewa kwa ufadhili wa kwanza, wavumbuzi ambao watakuwa wameonyesha uthibitisho wa dhana ya wazo lao, watakaokuwa wameunda mpango wa kupanuliwa na wenye uendelevu, na kuvutia ahadi kutoka kwa wadau wakuu na washirika, wanaweza kualikwa kutuma maombi ya ufadhili wa Programu ya Mpito hadi Upanuzi.

[1] Global Humanitarian Overview 2023 https://reliefweb.int/report/world/global-humanitarian-overview-2023-enaresfr

**SIKU YA MWISHO YA KUTUMA MAOMBI: Agosti 22, 2023, saa 14:00 ET.**

Akaunti zitakazofunguliwa baada ya tarehe na saa hii hazitashughulikiwa. Ikiwa tayari una akaunti ya Fluxx, hakuna haja ya kufungua akaunti tena.

Ili kutuma maombi ya ufadhili, watumaji maombi ya ufadhili LAZIMA watumie fomu ya maombi iliyotolewa mtandaoni, ambayo inapatikana TU kupitia tovuti ya Fluxx Grand Challenges Canada (gcc.fluxx.io). Watumiaji akaunti waliopo wanapaswa kuingia kwenye akaunti yao na watumiaji wapya lazima wafungue akaunti kwenye tovuti kuu ya programu kwenye Fluxx.  (tazama Sehemu ya 4.2 *Maagizo ya Kutuma Maombi*).

MUHIMU: Kwa sababu ya muda wa kushughulikia maombi yaliyotumwa, watumaji maombi LAZIMA wajisajili ili kupata akaunti ya Fluxx kabla ya tarehe 15 Agosti 2023.

Kwa usaidizi wa kiufundi kuhusu usajili wa akaunti au kutuma maombi ya miradi ya kufadhiliwa mtandaoni, wasiliana na timu ya Usaidizi wa Kiufundi ya Grand Challenges Canada Fluxx kwa http://www.grandchallenges.ca/fluxxsupport/

Kwa maswali yanayohusiana na Ombi hili la Kutuma Mapendekezo ya Miradi ya Kufadhiliwa ambayo hayajashughulikiwa kwenye sehemu ya Maswali Yanayoulizwa Sana, wasiliana na info@humanitariangrandchallenge.org

# YALIYOMO

**MUHTASARI MKUU** **0**
**1. UTANGULIZI** **3**
1.1 Utangulizi ....3
**2. MTAZAMO** **3**
2.1 Changamoto kuu ....3
2.2 Maeneo Lengwa ....4
2.3 Ufafanuzi wa Uvumbuzi ....7
2.4 Watu Walioathirika na Mzozo ....8
2.5 Ufadhili Uliopo ....9
2.6 Kulenga Matokeo ....9
2.7 Jukumu la Sekta ya Kibinafsi .... 10
2.8 Upanuzi na Uendelevu .... 11
2.9 Kile hatutafadhili .... 12
**3. SHUGHULI NA MATARAJIO** **12**
**4. SHERIA NA MIONGOZO** **13**
4.1 Vigezo vya Ustahiki .... 13
4.2 Maagizo ya Kutuma Maombi ya Ufadhili .... 14
4.3 Muda wa Kutuma maombi .... 17
4.4 Mchakato wa Ukaguzi .... 17
4.5 Vigezo vya Utathmini .... 18
4.6 Sheria na Masharti ya Fedha na Gharama Zinazostahiki .... 20
4.7 Masharti ya Malipo .... 20
4.8 Ukaguzi wa fedha .... 21
4.9 Gharama za kutuma maombi .... 21
**5. Sera na Masharti ya jumla** **21**
5.1 Hati za Uwasilishaji Maombi na Ilani ya Faragha .... 21
5.2 Udhamini .... 23
5.3 Mkakati wa Haki za Uvumbuzi na Kushiriki na Ufikiaji Wenye Athari .... 23
5.4 Sera ya Maadili na Uadilifu wa Utafiti .... 25
5.5 Kujitolea kwa Uendelevu wa Mazingira, Usawa wa Jinsia, na Haki za Kibinadamu .... 25
5.6 Haki za Grand Challenges Canada .... 26
5.7 Sheria Tawala .... 27
5.8 Usimamizi wa Hatari, Usalama, Kupambana na Ugaidi, Kupambana na Ufisadi na Kupambana na Rushwa .... 27
**KIAMBATISHO CHA A: KUWASILISHA MATOKEO** **29**

# 1. UTANGULIZI

### 1.1 UTANGULIZI

Katika mwongo uliopita, majanga ya aina mbalimbali - yanayotokana na mizozo, majanga ya asili, mabadiliko ya tabianchi, majanga ya kiuchumi, na misukosuko ya kijamii na kisiasa - yameongeza idadi ya watu wenye mahitaji ya usaidizi wa kibinadamu ambayo hayajatimizwa. Mwaka huu, zaidi ya watu milioni 339 wanahitaji msaada wa kibinadamu[2]. Licha ya kuongezeka kwa mahitaji ambayo hayajatimizwa, changamoto zinazoendelea katika utoaji wa misaada ya kibinadamu zinapunguza uwezo wa miundombinu ya misaada ya kimataifa kuwiana na hali halisi iliyopo.

Mashirika ya kimataifa ya misaada ya kibinadamu yanakabiliwa na changamoto katika kutoa misaada katika mazingira yaliyoathiriwa na mizozo, ikijumuisha kunyimwa ufikiaji, miundombinu iliyoharibiwa, kuingiliwa kisiasa, ubadhirifu wa misaada, ufisadi, changamoto zinazohusiana na huduma kufaa kijamii na kitamaduni, uratibu duni na vitisho vya vurugu. Watoa huduma wa maeneo husika mara nyingi huwa katika nafasi bora zaidi kufikia watu walioathirika katika mazingira yasiyo salama lakini hawana ufadhili na nyenzo za kufanya hivyo.

Kadiri kiwango cha dharura za kibinadamu kinavyoendelea kukua kwa kiwango kinachozidi uwezo wa mshirika mmoja au sekta yoyote kutoa mwitikio, na upungufu mkubwa wa ufadhili wa kibinadamu unamaanisha kuwa watoaji misaada ya kibinadamu wa kimataifa hawawezi kukidhi mahitaji yanayoongezeka, njia mpya na zilizoboreshwa za kufikiri na kufanya kazi pamoja ni muhimu.[3] Mashirika ya misaada, serikali, mashirika yasiyo ya serikali na sekta ya kibinafsi lazima yavumbue ili kuboresha ufaafu na ufanisi wa sekta ya kibinadamu, kuhamisha mamlaka hadi kwa watoaji huduma za kibinadamu mashinani, na kuunda upya mfumo mpana wa kushughulikia mapengo katika jinsi misaada inavyotolewa na jinsi juhudi za mwitikio zinatekelezwa.

*Kuleta Matumaini katika Mizozo: Ushirikiano katika Usaidizi wa Kibinadamu (CHIC)*), ushirikiano kati ya Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani, Ofisi ya Mambo ya Nje ya Uingereza, Jumuiya ya Madola na Maendeleo, Wizara ya Mambo ya Nje ya Uholanzi, Idara ya Masuala ya Kimataifa ya Canada, na Grand Challenges Canada, inalenga kutambua, kufadhili, kusaidia, na kuleta uvumbuzi mkubwa ambao unapunguza mateso na kuboresha maisha ya watu walioathiriwa na mizozo.

# 2. MTAZAMO

### 2.1 CHANGAMOTO KUU

[2] Muhtasari wa 2023 wa Misaada ya Kibinadamu Duniani https://reliefweb.int/report/world/global-humanitarian-overview-2023-enaresfr

[3] Ripoti ya SOHS ya ALNAP 2022 https://sohs.alnap.org/sites/alnap/files/content/attachments/2022-10-02/alnap-2022-sohs-report.pdf

Tunatafuta uvumbuzi thabiti, **unaookoa maisha au kuboresha maisha** ambao unakidhi vyema mahitaji ya watu walio hatarini zaidi na watu walioathiriwa na majanga ya kibinadamu yanayosababishwa na mizozo ambao vigumu kuwafikia. Uvumbuzi unaopendekezwa lazima uhusiane na mojawapo ya maeneo matatu yanayolengwa: 1) ufikiaji wa nishati, 2) habari muhimu za kuokoa maisha, au 3) bidhaa na huduma za afya. Tutavutiwa hasa na suluhisho ambazo zinashughulikia changamoto kuu kati ya maeneo haya yanayolengwa, yaliyoainishwa katika sehemu ya 2.2.

**Tunavutiwa sana kufadhili uvumbuzi unaomilikiwa na wenyeji.** Watu wanaoishi katika maeneo yenye mizozo na wale ambao wameathiriwa moja kwa moja na mizozo wako katika nafasi bora kushughulikia changamoto zao za kibinadamu. Kwa sababu ya maarifa ya muktadha na miunganisho yao kwa jamii zilizoathiriwa, watoa huduma wa ndani pia wako katika nafasi bora ya kufikia watu walioathiriwa katika mazingira yasiyo salama, lakini hawana ufadhili, rasilimali, au uwezo wa kutoa msaada katika maeneo ambayo ni magumu kufikiwa.

Maombi kutoka kwa watu walio nje ya jamii husika zilizoathiriwa lazima yaonyeshe jinsi suluhisho lao litakavyoarifiwa na tatizo la jamii husika, kupangwa pamoja na kutekelezwa kwa ushirikiano na jamii zilizoathiriwa na mizozo na/au watoa huduma za kibinadamu walio mashinani. Agizo letu la upendeleo katika suala la miunganisho aliyo nayo anayetuma maombi na jamii zilizoathiriwa ni kama ifuatavyo:

1. Shirika linalomilikiwa na jamii iliyoathiriwa - shirika ambalo timu za uongozi na utawala zinajumuisha zaidi watu binafsi wanaojitambulisha kuwa sehemu ya jamii iliyoathiriwa na mizozo inayowafikia na ambao wanaishi ndani au karibu na eneo lililoathiriwa na mizozo.
2. Wanaoongoza jamii zilizoathiriwa - angalau mtu mmoja katika nafasi ya usimamizi mkuu anatambulika kama anayetoka katika jamii iliyoathiriwa na mgogoro wanaotaka kutatua. Hawa pia wanaweza kuwa watu ambao wanaishi katika nchi za nje.
3. Ushirikiano wa jamii iliyoathiriwa - shirika lina makubaliano ya ushirikiano na usawa na mashirika ya kijamii yaliyo katika eneo lililoathiriwa na migogoro.

Kwa mwitikio wa jamii ambazo uwekezaji umekuwa mdogo kihistoria katika uvumbuzi unaoongozwa na wanawake,[4] pia tunatafuta kutoa upendeleo kwa timu ambazo mradi na/au uongozi wa shirika unajitambulisha kama mwanamke.

## 2.2 MAENEO LENGWA

Tangu 2018, CHIC imekuwa ikifadhili suluhisho anzilishi vumbuzi zinazolenga kushughulikia mahitaji makubwa zaidi ya watu walioathiriwa na migogoro katika maeneo matatu yafuatayo: (1) upatikanaji wa nishati; (2) ufikiaji wa habari msingi zinazookoa maisha; na (3) upatikanaji wa vifaa na huduma za afya. Maombi haya ya kuomba ufadhili (RFP) yanaitisha maombi mapya ya uvumbuzi mpya wa kushughulikia maeneo haya yanayolengwa.

[4] Ushirikiano Katika Usaidizi wa Kibinadamu (2021) Vizuizi vya Kisiasa na Kijamii katika Kupanua Uvumbuzi wa Usaidizi wa Kibinadamu

Ili kuboresha upatikanaji wa nishati; habari ya kuokoa maisha; au bidhaa na huduma za afya kwa jamii zilizoathirika, ubunifu unapaswa:

- Kushughulikia mojawapo ya vikwazo muhimu au changamoto kwa utoaji wa huduma zilizotambuliwa kwenye ukurasa wa 8 + 9.
- Kuhusisha maoni kutoka kwa watu walioathirika na mzozo wa kibinadamu.
- Kuonyesha uwezo wa kuzalisha athari zinazoweza kupimika na mabadiliko kwa maisha ya jamii zilizoathiriwa na mizozo.
- Kuonyesha uwezo wa kushiriki mfumo wa utoaji wa misaada ya kibinadamu katika njia mpya za kufanya kazi na kushawishi mabadiliko ya mifumo pana au mabadiliko[5] katika juhudi za usaidizi wa kibinadamu.[6]

Tathmini ya hivi karibuni ya programu hii ilithibitisha kuwa maeneo ya mada zinazolengwa za CHIC yanafaa kwa jamii zilizoathiriwa na mizozo, wavumbuzi, na waundaji sera za usaidizi wa kibinadamu. Utafiti wa ufuatiliaji wa baadaye umefanywa ili kuthibitisha zaidi na kutambua vikwazo maalum au changamoto chini ya kila mojawapo ya maeneo matatu yanayolengwa. Maelezo yafuatayo yanaelezea aina za vizuizi tunavyolenga kushughulikia na aina za suluhisho tunazovutiwa nazo:

**Ufikiaji wa Nishati**

***Ubunifu unaowezesha upatikanaji sawa na wa bei nafuu kwa suluhisho za mabadiliko ya tabianchi na/au bidhaa au huduma za nishati mbadala kwa watu walio katika mazingira magumu zaidi walioathirika na mizozo.***

- Nishati ya sekta ya umma haipatikani na suluhisho za nishati mbadala za sekta binafsi zinaweza kuwa hazipatikani kwa watu walio katika hali ngumu zaidi katika mazingira yaliyoathiriwa na mizozo.
- Bila mifano ya biashara endelevu, mifumo mpya ya nishati haina matengenezo ya kutosha na huharibika. Hii inasababisha utoaji duni wa huduma.
- Suluhisho mpya zinahitajika ambazo zinazingatia vipengele kama vile utoaji sawa wa huduma, mifano endelevu ya mapato, na/au mifano bora ya ruzuku ili kukidhi mahitaji ya nishati ya watu walio katika mazingira magumu zaidi.

**Habari za kuokoa maisha**

***Uvumbuzi unaoboresha uaminifu na usalama wa habari muhimu au za kuokoa maisha*** *na****/au kuboresha mawasiliano ya njia mbili.***

[5] *Mabadiliko ya mifumo hufafanuliwa kama kubadilisha mifumo ya msingi ambayo misaada wa kibinadamu hutolewa, na hivyo kuathiri uhusiano na mienendo ya uongozi, na maadili na kanuni zilizoshikiliwa kwa kina. Kwa mfano, kuendeleza mchakato mpya, bidhaa au mbinu mpya ambayo inahimiza mabadiliko ya kimuundo kuelekea uundaji wa bidhaa za misaada badala ya kuagiza bidhaa zilizoundwa tayari, na hivyo kubadilisha uzalishaji kutoka kwa mfumo wa jadi wa usambazaji wa bidhaa za msaada wa kibinadamu na kuwezesha masoko ya ndani na watu.*

[6] Uwezo huu huenda hautatimizwa kikamilifu wakati wa kipindi cha ufadhili wa kwanza, lakini unapaswa kuwa na uwezo wa kuonyesha hamu ya uvumbuzi wako miongoni mwa wadau wafaao katika mfumo wa utoaji misaada ya kibinadamu.

- Upatikanaji wa taarifa za kuaminika na salama zinazosambazwa kwa njia ya dharura au taarifa za "kuokoa maisha" ni changamoto iliyoenea katika mazingira yaliyoathiriwa na mizozo.
- Mawasiliano sahihi ya njia mbili kati ya jamii zilizoathirika na wahojiwa wa kibinadamu mara nyingi ni magumu kufikia, hali ambayo inaweza husababisha kutoaminiana na kuchanganyikiwa na majibu ya jumla.
- Suluhisho zinahitajika ili kuwezesha ufikiaji wa wakati unaofaa/wa kuaminika kwa habari muhimu, wakati wa kuhakikisha hatua za kutosha za usalama wa data na faragha ziko mahali pa kulinda walio hatarini zaidi.
- Suluhisho ambazo zinaunganisha sauti, maoni na majibu ya jamii zilizoathiriwa katika hatua zote za juhudi za usaidizi wa kibinadamu.
- Huku tukivutiwa na suluhisho ambazo zinajumuisha matumizi ya utashi wa akili na/au kufundisha mashine, tunavutiwa zaidi na suluhisho zinazoonyesha uzingatiaji wa kutosha na matumizi ya kanuni zisizo na madhara katika matumizi ya teknolojia kama hizi.[7]

**Bidhaa na huduma za afya**

***Uvumbuzi unaoshughulikia vizuizi vinavyohusiana na miundombinu duni ya huduma za afya, ujuzi wa wafanyakazi wa afya, na mapungufu ya ufuatiliaji wa magonjwa yaliyopo na majibu yaliyopo.***

- Vituo vya huduma za afya havipati rasilimali za kutosha, vimo katika hatari ya kushambuliwa, havina matengenezo ya kutosha ya vifaa, na vina ufikiaji mdogo wa teknolojia ya usimamizi wa huduma za afya. Teknolojia za kusaidia watu wenye ulemavu hazipatikani.
- Wafanyakazi wa huduma za afya - wote rasmi na wasio rasmi - huenda wanahitaji msaada wa kuimarisha uwezo ili kushughulikia magonjwa mapya na tofauti na majeraha yanayotokea katika mazingira ya usaidizi wa kibinadamu.
- Suluhisho mpya zinahitajika ili kushughulikia mapungufu katika ufuatiliaji wa/na kukabiliana na magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza (ikiwemo masuala ya afya ya akili) katika mazingira yaliyoathiriwa na mizozo.
- *Tunavutiwa hasa na suluhisho zinazohusiana na afya ambazo zinazingatia uhusiano kati ya mabadiliko ya tabianchi na afya (kwa mfano, matumizi ya nishati mbadala, upunguzaji/utupaji salama wa taka za matibabu).*

**Mada Zinazoingiliana**

***Suluhisho za kiwango cha mifumo***

Katika maeneo yote matatu yanayolengwa, tutapendelea uvumbuzi ambao, mbali na kuathiri maisha ya jamii zilizoathirika, una uwezo wa kuleta ushawishi mkubwa wa kiwango cha mifumo au mabadiliko katika njia ambazo msaada wa kibinadamu hutolewa.

---

[7] https://international-review.icrc.org/articles/harnessing-the-potential-of-artificial-intelligence-for-humanitarian-action-919

Matatizo ambayo uvumbuzi wa sekta ya usaidizi wa kibinadamu unatafuta kushughulikia ni changamano, yana sura nyingi na yanaweza kupanuka zaidi ya muundo wa kiufundi wa suluhisho. Kwa kuzingatia hili, CHIC inawahimiza wavumbuzi kujizamisha ndani ya mfumo wa watoaji misaada ya kibinadamu, jamii zilizoathiriwa, mamlaka za mitaa na wadau wengine muhimu. Huku ikitambulika kuwa hakuna uvumbuzi mmoja unaoweza kubadilisha mfumo peke yake, uwazaji wa makini na kufanya kazi kwa uwazi wa mifumo kunaweza kufanya kila uvumbuzi kuwa nguvu ya mabadiliko.

Mabadiliko ya mifumo hufafanuliwa kama kubadilisha mifumo ya msingi ambayo misaada ya kibinadamu hutolewa, na hivyo kuathiri uhusiano na mienendo ya uongozi, pamoja na maadili na kanuni zilizoshikiliwa kwa kina. Kwa mfano, kuendeleza mchakato mpya, bidhaa au mbinu mpya ambayo inahimiza mabadiliko ya kimuundo kuelekea uundaji wa bidhaa za misaada badala ya kuagiza bidhaa zilizoundwa tayari, na hivyo kubadilisha uzalishaji kutoka kwa mfumo wa jadi wa usambazaji wa bidhaa za msaada wa kibinadamu na kuwezesha masoko ya ndani na watu. Mara nyingi, mabadiliko ya mifumo yanahitaji mchanganyiko wa uvumbuzi wa bidhaa au [8]uvumbuzi wa michakato ili kuafikiwa kikamilifu.

***Ujanibishaji na Kubadilisha mamlaka***
Mfumo wa uvumbuzi wa kibinadamu unaonyesha mfumo wa kibinadamu wenyewe: kiwango kikubwa cha ukosefu wa usawa, kinachoambatana na uongozi na ufadhili ambao bado umejikita katika kaskazini ya ulimwengu, na wavumbuzi kutoka kusini mwa ulimwengu wanakabiliwa na vikwazo vikubwa vya kupata mtaji wa uwekezaji na kuongeza uvumbuzi. Katika kukabiliana na hili, tutatoa kipaumbele kwa ufadhili wa uvumbuzi unaomilikiwa na wenyeji ambao wako karibu na wale walioathirika na migogoro, na unaoweza kuonyesha faida za mbinu zaidi za mashinani za kukabiliana na migogoro ya kibinadamu.

Pia tunahimiza uvumbuzi unaoweza kuunganisha mada zifuatazo zinazoingiliana (mada zimefafanuliwa zaidi katika sehemu ya 5.5):

- Usawa wa kijinsia
- Ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi
- Ushirikiano na uwezeshaji wa jamii

Mapendekezo yanayoonyesha umuhimu wa, au kutambua fursa za uwezekano wa, ushirikiano na sekta ya kibinafsi pia yanahimizwa.

*Kulingana na ubora wa mapendekezo yatakayopokewa, Humanitarian Grand Challenge ina haki ya kupunguza lengo hadi mojawapo au maeneo zaidi yaliyo hapo juu. Mapendekezo yanayoshughulikia sekta zaidi ya moja yanakaribishwa sana.*

## 2.3 Ufafanuzi wa Uvumbuzi

[8]**Uvumbuzi wa bidhaa** hurejelea bidhaa mpya au zilizoboreshwa ili kuimarisha misaada ya kibinadamu. **Uvumbuzi wa mchakato** hurejelea ubunifu unaobadilisha au kuboresha michakato ambayo bidhaa / huduma zinatengenezwa/kuwasilishwa.

Tunafafanua uvumbuzi kama mawazo ya ujasiri yenye uwezo wa kubadilisha kimsingi jinsi suluhisho za kuokoa maisha na kuboresha maisha zinafikia na kusaidia watu walio katika mazingira magumu zaidi walioathirika na mizozo. Uvumbuzi unamaanisha kukabiliana na tatizo kwa njia mpya na tofauti ikilinganishwa na juhudi zilizopo.

Ufafanuzi wetu wa uvumbuzi ni pamoja na kujaribisha mawazo yaliyopo katika miktadha mipya. Wazo ambalo linafanya kazi katika muktadha thabiti ambalo halijawahi kujaribiwa katika mazingira ya mgogoro linaweza kuzingatiwa kwa ufadhili. Katika hali kama hizi, suluhisho lazima lionyeshe uelewa wa mazingira ya mizozo na liwe na uwezo wa kushughulikia kizuizi mahususi, kilichopo ambacho kinapunguza usaidizi wa kibinadamu katika maeneo ya mizozo huku likidumisha kanuni za usaidizi wa kibinadamu.

**Uvumbuzi Jumuishi**

Miradi inatarajiwa kuchukua mtazamo wa Uvumbuzi Jumuishi®, unaofafanuliwa kama matumizi ya uratibu wa uvumbuzi wa kisayansi/kiteknolojia, kijamii na biashara ili kuunda suluhisho kwa changamoto ngumu. Mtazamo huu haupuuzi faida za kila mojawapo ya aina hizi za uvumbuzi peke yake, bali unaangazia ushirikiano wenye nguvu ambao unaweza kupatikana kwa kuunganisha uvumbuzi katika sehemu hizo tatu. Kwa maelezo zaidi, tafadhali tazama: www.grandchallenges.ca/integrated-innovation .

### 2.4 WATU WALIOATHIRIKA NA MZOZO

Humanitarian Grand Challenge inalenga zaidi kukidhi mahitaji ya watu ambao ni vigumu kufikiwa kutokana na dharura za usaidizi wa kibinadamu zinazosababishwa na mizozo. Upendeleo wetu katika suala la watu walioathirika ni kama ifuatavyo:

1. Watu ambao kwa sasa wanaishi katika maeneo yenye mizozo
2. Wakimbizi wa ndani kwa ndani
3. Wakimbizi[9]

Tunavutiwa na uvumbuzi unaofaa mazingira ya kambi, mijini, na vijijini.

Tunahimiza uvumbuzi unaoshughulikia mahitaji ya wanawake na wasichana, na watu ambao wametengwa kijamii kwa sababu ya jinsia zao, utambulisho, ujinsia, dini, umri au mapato, pamoja na watu wenye ulemavu, watu wachache katika jamii na watu wasio na utaifa.

Muktadha ambao tunazingatia kuwa maeneo magumu ya kufikia mizozo unajumuisha, bila kuacha nje:

- Jamhuri ya Afrika ya Kati
- Ethiopia (eneo la Tigray)
- Iraq
- Libya

[9]Hii inaweza pia kujumuisha, kwa ujumuishaji, misaada kwa jamii wenyeji zilizo katika mazingira magumu.

- Mali
- Msumbiji (Cabo Delgado na Nampula)
- Nigeria (maeneo ya kaskazini)
- Somalia
- Sudani
- Sudani ya Kusini
- Syria
- Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (eneo la Kivu)
- Yemen

CHIC imejitolea kuunga mkono suluhisho zinazolenga kupunguza au kubadilisha athari mbaya za mabadiliko ya tabianchi kwa watu walio katika mazingira magumu, walioathirika na mizozo na kutambua athari mabadiliko ya tabianchi yanaweza kuwa nayo kwa mienendo ya mizozo na uhamishaji wa watu wengi. Tunakaribisha suluhisho ambazo zinasaidia jamii zilizoathiriwa na mizozo ambazo pia zinaathiriwa na mabadiliko ya tabianchi.

Kumbuka: Kwa sababu ya sheria za sasa za Serikali ya Canada, kwa wakati huu, hatuwezi kukagua suluhisho zinazotekelezwa nchini Afghanistan. Kupata maelezo zaidi, angalia: https://www.canada.ca/en/public-safety-canada/news/2023/03/bill-c-41-an-act-to-amend-the-criminal-code-and-to-make-consequential-amendments-to-other-acts.html

## 2.5 UFADHILI ULIOPO

**Ufadhili wa Kwanza**

Lengo la ufadhili huu wa kwanza ni kujaribisha mawazo mapya na suluhisho zilizoboreshwa za kushughulikia changamoto za usaidizi wa kibinadamu ili kuamua ikiwa zina ufanisi au la. Kufikia mwisho wa kipindi cha ufadhili, miradi itakayopokea ufadhili wa kwanza inatarajiwa kuonyesha ushahidi unaoweza kupimika (kwa mfano, ushahidi wa utekelezaji wa dhana yao), katika mazingira yaliyodhibitiwa au finyu, kwamba suluhisho lililopendekezwa ni bora na/au linafaa zaidi kuliko mbinu zilizotumika awali za misaada za kibinadamu na kwamba uvumbuzi una uwezo wa kuendelezwa na kupanuliwa zaidi.

Kupitia Ombi hili la Mapendekezo, Humanitarian Grand Challenge itatoa ufadhili wa kwanza kufikia $250,000 CAD kwa mradi kwa muda wa miezi ishirini na nne (24) kuanzia Aprili 2024. Mbali na ufadhili, watakaopewa ufadhili wanaweza kupokea msaada wa ziada, kama vile msaada wa jumla wa kuongeza kasi, fursa za ushauri, na upatikanaji wa hafla za kujenga mahusiano.

Tunatarajia kutoa hadi misaada ya kwanza 20 kupitia Ombi hili la Mapendekezo. Mwishoni mwa kipindi ya ufadhili wa kwanza, uvumbuzi ambao umefikia Uthibitisho wa Dhana unaweza kualikwa kuomba Ufadhili Mpito kwa Fedha za Kuendeleza dhana.

## 2.6 KULENGA MATOKEO

Matokeo ya mwisho ya Humanitarian Grand Challenge ni **maisha yaliyookolewa na maisha kuboreshwa** kwa watu walioathirika na mizozo.

Mifano ya jinsi CHIC inavyofafanua maisha yaliyoboreshwa katika maeneo tofauti yanayolengwa:

- **Afya:** kupunguza magonjwa kwa njia ya kuzuia au kutibu ugonjwa au tatizo la afya
- **Nishati:** matumizi ya kawaida, thabiti ya chanzo cha nishati imara na cha kuaminika
- **Habari ya kuokoa maisha:** matumizi ya kawaida, thabiti ya chanzo cha habari za kuaminika na sahihi

Matokeo ya kitakwimu na ya kimaelezo, kama vile viashiria vya faida na gharama kwa mfano, yanapaswa pia kukusanywa ili kuonyesha athari za uvumbuzi.

Kwa kuzingatia kuwa athari halisi za uvumbuzi zinapatikana katika siku zijazo, mapendekezo lazima yajumuishe mpango wa jinsi viashiria vya matokeo ya haraka na ya kati vitafuatiliwa na kutathminiwa kwa kipindi cha mradi.

Wavumbuzi wanapaswa kuonyesha kujitolea kushiriki masomo waliyojifunza na mifumo ya usaidizi wa kibinadamu - mafanikio na changamoto. Kulingana na ufadhili, tunakusudia kuleta wavumbuzi waliofanikiwa pamoja ili kushiriki masomo waliyojifunza mara kwa mara.

**Kuwasilisha Matokeo**

Kuwasilisha matokeo ni sehemu muhimu ya uwajibikaji wa mradi kwa washirika wa Humanitarian Grand Challenge na wadau wengine muhimu. Wavumbuzi wanapaswa kuzingatia jinsi matokeo yatasambazwa ili kuendesha athari za uvumbuzi na maendeleo kuelekea kiwango cha upanuzi na uendelevu.

Kwa maelezo zaidi tazama Kiambatisho cha A.

### 2.7 Jukumu la Sekta ya Kibinafsi

Kutokana na kiwango cha sasa cha mahitaji ya kibinadamu, changamoto hii ni kubwa sana kwa sekta moja kutatua peke yake. Mitazamo ya sekta ya kibinafsi ya kufanya majaribio, kuongeza kasi katika utekelezaji wa suluhisho endelevu, kuboresha kasi, ubora na upunguzaji gharama za utengenezaji bidhaa na huduma, uchakataji bidhaa na kufadhili suluhisho zenye uvumbuzi inaweza kuzalisha suluhisho bora zaidi na zenye athari nzuri kwa jamii. Sekta ya kibinafsi inaweza kuchangia utaalamu muhimu wa kiufundi, usimamizi wa hatari, na ufikiaji wa mitandao na data, na mara nyingi inaweza kuwa na ujuzi wa kina kuhusu hali za ndani na mashinani. Kwa mfano, biashara ndogo ndogo za mitaa mara nyingi ni muhimu katika kutoa bidhaa za kuokoa maisha na kuboresha maisha baada ya vita vya silaha. Wavumbuzi wanahimizwa kunufaika na ujuzi wa kimsingi wa sekta ya kibinafsi katika miradi yao au kushirikiana na sekta ya kibinafsi ili kuongeza athari za uvumbuzi wao, pale inapofaa.

Ili kupokea ufadhili wa kwanza, watumaji maombi ya ufadhili wanahimizwa kuonyesha umuhimu wa suluhisho kwa, au kutambua fursa za uwezekano wa, ushirikiano na sekta ya kibinafsi. Maombi ya ufadhili wa kwanza yanaweza kuonyesha uhusiano unaowezekana na sekta ya kibinafsi kwa (lakini sio tu uhusiano huo): kujadili mshirika wa sasa au anayewezekana kutoka

sekta ya kibinafsi, mtazamo wa soko, au mabadiliko ya baadaye ya suluhisho hadi suluhisho la mashinani, biashara endelevu au soko.

Sekta ya kibinafsi inafafanuliwa kama taasisi/mashirika/biashara za faida katika ngazi ya ndani, kitaifa au kimataifa, na hurejelea mashirika na washiriki wafuatao:

- Mashirika ya kibinafsi ya faida, kama vile biashara, shirika, au kampuni ya kibinafsi
- Taasisi ya kibinafsi au taasisi za kifedha za kibinafsi, ikijumuisha makampuni binafsi ya uwekezaji, fedha za pamoja au makampuni ya bima
- Wawekezaji wa kibinafsi (watu binafsi au makundi)
- Biashara za kibinafsi au mashirika ya sekta, ikijumuisha na sio tu taasisi za biashara na aina za taasisi zinazohusiana na biashara na mashirika haya
- Wakfu binafsi zinazotoa ufadhili au taasisi za uhisani.

Ujumuishaji wa sekta ya kibinafsi katika maombi unaweza kuwa kupitia ushiriki wa kifedha au wa uhisani, au ushirikiano.

Taasisi za sekta ya kibinafsi pia zinahimizwa kuomba ufadhili huu.

### 2.8 Upanuzi na Uendelevu

Kwa Humanitarian Grand Challenge, uendelevu unarejelea uwezo wa uvumbuzi uliofanikiwa kutumiwa kwa urahisi katika miktadha ya sasa na ya baadaye, na upanuzi unarejelea uwezo wa uvumbuzi uliofanikiwa kufikia idadi kubwa ya watu ambao watafaidika kadri iwezekanavyo. Mapendekezo yanapaswa kufafanua kwa ushawishi jinsi miradi yao itakavyoendelea kufikia upanuzi na uendelevu. Wavumbuzi wanapaswa kutumia fedha za ufadhili wa kwanza kujaribisha mbinu za upanuzi na uendelevu na lazima wawe na mpango thabiti na dhana iliyothibitishwa ili kupokea ufadhili wa mpito wa kuendeleza mradi.

**Uelewa wa Majanga Yanayosababishwa na Mizozo**
Ili kusaidia wote kuhakikisha athari endelevu katika kiwango cha upanuzi na kwamba miradi inayopendekezwa inakidhi mahitaji ya ndani na haiongezei mivutano wa kisiasa, kijamii, na kiuchumi, ni muhimu kwamba timu za mradi zijumuishe watu binafsi wenye uelewa wa muktadha wa kijamii, kisiasa na kiuchumi. Kwa kufanya hivyo, miradi inaweza kushughulikia vyema mahitaji ya watu walioathirika na kutambua hatari kwa mafanikio ya mradi.

**Ushirikishi wa Wadau**
Watu walioathirika na mizozo na wale ambao hatimaye watafanya maamuzi kuhusu matumizi ya suluhisho, kama vile mashirika ya usaidizi wa kibinadamu (mitaa, kitaifa au kimataifa), mashirika ya Umoja wa Mataifa, mashirika ya Msalaba Mwekundu au watoa huduma za usaidizi wa kibanadamu wengine wasio wa kawaida (makundi ya kidini, vikundi vya jamii za mitaa, sekta binafsi) wanatarajiwa kushiriki mwanzoni na katika kipindi chote cha mradi. Maoni na ushiriki wa aina hizi za mashirika katika kipindi kizima cha mradi ni muhimu kwani watahusika katika awamu ya tathmini ya mchakato. Hii itasaidia kuhakikisha kuwa suluhisho itaweza kutumiwa mwanzoni na marekebisho kwa ajili matumizi ya baadaye, hali

inayozalisha athari kubwa. Zaidi ya hayo, wadau wanaweza kutoa maarifa ya suluhisho kwa jamii zao na kutambua mambo muhimu yanayohitajika kwa ufanisi wa mradi.

### 2.9 KILE HATUTAFADHILI

1. Uvumbuzi ambao haulengi muktadha unaohusiana na mizozo na migogoro
2. Mitazamo ambayo hutumia ufuatiliaji unaohusiana na usalama, silaha, nguvu au teknolojia sawia. Pendekezo lolote la matumizi ya droni lazima likaguliwe kwa uangalifu katika mchakato changamano na linapaswa kufuata UAV Code of Conduct.
3. Sayansi ya ugunduzi, mipango ya kujenga uwezo tu, ufadhili unaoendelea wa programu au maendeleo ya miundombinu.
4. Miradi inayohusisha kuanzisha ushahidi wa dhana ya uvumbuzi ambayo haki za msingi za mali ya kiakili zinamilikiwa na taasisi nyingine, isipokuwa: (a) taasisi hiyo imempa mtumaji maombi haki za kutosha za leseni za uvumbuzi ili kuruhusu upanuzi katika nchi zinazofaa, au (b) taasisi hiyo iko tayari kutia saini ahadi ya Grand Challenges Canada ya kujitolea kuzingatia Sera ya Global Access. https://www.grandchallenges.ca/wp-content/uploads/2019/03/Global-Access-Policy_March-5-2019_ENG.pdf

Vigezo vyote vinaweza kubadilika wafadhili wapya wakijiunga na Changamoto hii; sasisho zitachapishwa kwenye sehemu ya "Maswali Yanayoulizwa Sana" ya tovuti ya Humanitarian Grand Challenge website.

# 3. SHUGHULI NA MATARAJIO

Wavumbuzi wanaofadhiliwa chini ya mpango huu watatarajiwa kushiriki katika shughuli zifuatazo na kutoa vigezo maalum vinavyohitajika vilivyoorodheshwa hapa chini ili kuonyesha maendeleo ya mradi na mafanikio:

1. Ripoti ya utendaji inayolenga matumizi ya fedha na matokeo yaliyoafikiwa. Kasi ya kutoa ripoti itakuwa kila baada ya miezi mitatu au sita, kulingana na tathmini yetu ya hatari ya mradi na taasisi.

2. Usambazaji wa maarifa kwa wakati unaofaa, ikiwemo kupitia mitandao ya kijamii, machapisho ya ufikiaji huru wa habari usiotozwa, kulinda data yenye vitambulisho vya watu binafsi katika hazina zinazopatikana kwa umma, matangazo ya vyombo vya habari, makongamano, ushiriki wa wadau, n.k. Kutambuliwa kwa washirika wa Humanitarian Grand Challenge kutahitajika.

3. Ripoti ya mwisho inayohesabu matumizi ya fedha na ambayo inafanya tathmini ya wazi ya athari za mradi. Tafadhali kumbuka kuwa 5% ya kushikilia sehemu ya fedha itatumika kwa fedha zote chini ya mpango huu, kisha itatolewa kwa wavumbuzi baada ya kuwasilisha ripoti ya mwisho ya kuridhisha na uthibitishaji wa gharama zote.

4. Sasisho za athari za baada ya ufadhili kuendelea, ufikiaji wa kimataifa, upatikanaji wa data, na usimamizi wa hakimiliki katika uvumbuzi uliofadhiliwa.

Maelekezo ya kuripoti yatatolewa kwa wapokeaji ufadhili waliofanikiwa. Ripoti za maendeleo zilizoandikwa na mazungumzo kupitia mikutano ya simu zinaweza kuhitajika ili kukidhi mahitaji ya kuripoti.

Mbali na shughuli zilizotajwa hapo juu, wavumbuzi watatarajiwa:

- Kushiriki katika shughuli za kuhusisha umma.
- Kuchangia ajenda ya kujifunza kwa changamoto mahususi, ikiwemo kushiriki katika mikutano na matukio

Wavumbuzi waliofadhiliwa lazima wahifadhi nyaraka za mradi zinazofaa, ikijumuisha rekodi za kifedha, na zinazoweza kukaguliwa na Grand Challenges Canada, Idara ya Masuala ya Kimataifa ya Canada, Wizara ya Mambo ya Nje ya Uholanzi, UK FCDO, na / au USAID wakati wowote hadi Septemba 30, 2030; Mahitaji yanayohusiana yataonyeshwa katika mikataba ya ufadhili.

# 4. SHERIA NA MIONGOZO

Mapendekezo yatakayowasilishwa yatapitia mchakato wa ukaguzi wa hatua nyingi kabla ya Kamati ya Uendeshaji ya Humanitarian Grand Challenge [10]kutoa mapendekezo ya ufadhili. Bodi ya Wakurugenzi ya Grand Challenges Canada itafanya maamuzi ya mwisho ya ufadhili. Kwa maelezo zaidi kuhusu Bodi ya Wakurugenzi: https://www.grandchallenges.ca/governance/.

## 4.1 VIGEZO VYA USTAHIKI

1. Watumaji maombi ya ufadhili wanaostahiki ni pamoja na makampuni ya kijamii na taasisi nyingine zinazotambuliwa (kwa mfano, mashirika yasiyo ya faida na makampuni ya faida) ambayo

    - yameundwa na kuanzishwa kisheria
    - yanaweza kufanikiwa kutekeleza shughuli katika eneo lao la kiufundi
    - yanaweza kupokea na kutekeleza ufadhili huu.

    Biashara ya mtu mmoja haistahiki kupata ufadhili huu.

    Katika uzoefu wetu wa awali, tumegundua kuwa mashirika ya kimataifa kama vile Umoja wa Mataifa kwa kawaida hayawezi kukubaliana na sheria na masharti ya mikataba yetu ya ufadhili. Tunapendekeza sana kwamba mashirika haya badala yake yatume maombi kupitia shirika linalostahiki. Wafanyakazi kutoka ofisi ya Umoja wa Mataifa wanaweza kuwa washirika katika mradi huo.

2. Mradi unaweza kuwa na Kiongozi mmoja tu wa Mradi, ambaye lazima awe na uhusiano na taasisi inayowasilisha pendekezo.

[10]Kamati ya Uendeshaji Shindano la Humanitarian Grand Challenge inajumuisha USAID, UK FCDO, Wizara ya Mambo ya Nje ya Uholanzi, Masuala ya Kimataifa ya Canada na Grand Challenges Canada.

3. Kiongozi wa Mradi anaweza kuorodheshwa tu kwenye programu moja (1) kwa Ombi hili la Mapendekezo. Taasisi inaweza kuwa mtumaji maombi ya ufadhili kwenye mapendekezo mengi, mradi maombi yote yana Viongozi tofauti wa Mradi.

4. Maombi lazima yajumuishe habari zote zinazohitajika. Ni maombi kamili tu ndiyo yatazingatiwa na Kamati ya Ukaguzi.

5. Washirika wa Humanitarian Grand Challenge wanaweza, wakati wowote na kwa hiari yao pekee, kurekebisha vigezo vya ustahiki kwa heshima ya watumaji maombi binafsi, Viongozi wa Mradi na/au nchi zinazostahiki, kwa kiwango ambacho marekebisho hayo hayadhoofishi mchakato wa ukaguzi.

**Tafadhali kumbuka** kuwa Grand Challenges Canada lazima iidhinishe mabadiliko yoyote katika shirika linalotuma maombi au Kiongozi wa Mradi, kutoka kwa maombi ya awali**.**

### 4.2 MAAGIZO YA KUTUMA MAOMBI YA UFADHILI

**Kuwasilisha maombi ya ufadhili**

**Ili kutuma ombi la mradi wa kufadhiliwa, waomba ufadhili lazima watumie programu ya mtandaoni iliyotolewa, ambayo inapatikana tu kupitia Tovuti ya Grand Challenges Canada Fluxx**. **(**https://gcc.fluxx.io**). LAZIMA ufungue akaunti kufikia Agosti 16, 2023 saa 6:59 Asubuhi Saa za Afrika Mashariki (6:59 EAT).**

Grand Challenges Canada **haiwezi** kutoa maswali ya kutuma ombi kupitia baruapepe na maombi ya miradi ya kufadhiliwa yaliyowasilishwa kupitia baruapepe hayashughulikiwa. Kivinjari kinachopendekezwa ni Google Chrome (USITUMIE Internet Explorer).

**Tafadhali kumbuka:** Ni lazima maombi ya miradi ya kufadhiliwa yawasilishwe kwa kutumia akaunti ya mtu binafsi anayestahiki na shirika/taasisi inayostahiki. Ombi likishatumwa, maelezo kutoka kwa akaunti iliyotumiwa yataonyeshwa (kwa mfano Kiongozi wa mradi na taasisi ya kutuma ombi) kwenye fomu ya maombi ya ufadhili; haya hayawezi kubadilishwa bila kuwasiliana na Grand Challenges Canada. Ni maombi yaliyowasilishwa tu na akaunti ambayo ilitimiza vigezo vya kustahiki ndiyo yatashughulikwa na kukaguliwa.

1) Nenda kwenye https://gcc.fluxx.io

   *Watumiaji akaunti waliopo:*
   a) Ikiwa ulituma ombi la ufadhili wa mradi hapo awali, **tayari** una akaunti na huhitaji kufungua akaunti mpya.
   b) Ikiwa hukumbuki nenosiri lako, unaweza kulibadilisha ili ufikie Fluxx haraka – bonyeza tu kwenye kiungo cha *Badilisha* au *Unda Nenosiri Jipya*.
   c) Ikiwa anwani yako ya baruapepe au ushiriki wako wa shirika umebadilika tangu ulipojisajili hapo awali, utahitaji kufungua akaunti mpya.

   *Watumiaji wapya:*
   a) Ikiwa wewe ni mtumiaji mpya, bonyeza kitufe cha *Unda akaunti*. Itachukua angalau siku moja (1) ya kazi lakini inaweza kuchukua hadi siku tatu (3) za kazi,

kushughulikia ombi lako. Hakikisha umefanya hivi haraka iwezekanavyo, ili uwe na muda wa kutosha wa kukagua na kukamilisha ombi lako la ufadhili.

  b) Maelezo yako yakishashughulikiwa, utatumiwa jina la mtumiaji na kiungo cha URL ili uweke nenosiri utakalochagua. Usipopokea baruapepe yako ya kuingia katika akaunti, tazama folda yako ya taka/spam. Bonyeza kwenye kiungo cha URL kilichotolewa kwenye baruapepe ili uweke nenosiri utakalochagua.

2) Ukishapata maelezo ya akaunti yako, ingiza jina lako la mtumiaji na nenosiri. Bonyeza *Ingia.*
3) Bonyeza kwenye kiungo cha *Karibu/Bienvenue/Welcome* kwenye menyu ya kushoto, kisha enda kwenye sehemu ya Kuleta Matumaini katika Mizozo: Ushirikiano katika Usaidizi wa Kibinadamu, bonyeza kitufe cha *Tuma Ombi la Ufadhili wa Mradi.*
   a) Unaweza *Kuhifadhi* kazi yako wakati wowote na kuirudia baadaye kwa kuingia katika akaunti yako na kubonyeza *Rasimu*, kisha kubonyeza *Hariri.*
   b) Ukimaliza kuhariri, hifadhi fomu yako na ubofye kitufe cha *Wasilisha*. Ukishawasilisha, hutaweza tena kuhariri au kubadilisha ombi lako.
   c) **LAZIMA utume ombi lako kupitia Fluxx kabla ya tarehe 22 Agosti 2023 saa 9:00 Usiku Saa za Afrika Mashariki.**

Hatua zilizo hapo juu (pamoja na picha za skrini) zimefafanuliwa katika **Mwongozo wa Marejeleo ya Haraka wa Fluxx.** Mwongozo wa Marejeleo ya Haraka wa Fluxx unaeleza jinsi ya kufungua akaunti ya Fluxx, jinsi ya kuweka upya nenosiri kwenye akaunti iliyopo na vidokezo vingine muhimu vya kutumia Fluxx na fomu ya maombi ya ufadhili wa mradi. Ikiwa bado unahitaji usaidizi wa kiufundi kuhusu kufungua akaunti au kutuma maombi ya mtandaoni, unaweza pia *Kuwasilisha Tiketi.* Tafadhali tembelea https://www.grandchallenges.ca/fluxxsupport/ ili kufikia **Mwongozo wa Marejeleo ya Haraka wa Fluxx** na/au *Kuwasilisha Tiketi* kwa Timu ya Usaidizi wa Kiufundi ya Fluxx ya Grand Challenges Canada.

Ikiwa una swali kuhusu programu, usitume baruapepe kwa Timu ya Usaidizi wa Kiufundi ya Tovuti ya Jamii, tafadhali kwanza rejelea hati ya “Maswali Yanayoulizwa Sana ” na kisha uwasiliane na info@humanitariangrandchallenge.org.

Watumaji maombi ya ufadhili wataulizwa kujibu mfululizo wa maswali kuhusu wazo lao la uvumbuzi, lengo, madhumuni na shughuli, mtazamo, mfumo wa kupima mafanikio, na bajeti - angalia Kiambatisho B kwa muhtasari wa kutuma maombi ukiwa nje ya mtandao.

**Zana za Mvumbuzi**

Watumaji maombi ya ufadhili wanahimizwa kufikia Zana za Mvumbuzi za Grand Challenge Canada katika grandchallenges.ca/innovator-toolbox, ambayo ina makala ya kusaidia watafiti na wavumbuzi kuunda mapendekezo yao ya mradi na kupanga jinsi uvumbuzi wao utapanuliwa, kuwa endelevu na kuwa na athari za kimataifa. Pia tazama Tovuti ya Usawa wa Jinsia katika grandchallenges.ca/gender kwa seti ya zana za usawa wa kijinsia.

**Maswali**

Tafadhali kwanza rejelea sehemu yetu ya "Maswali Yanayoulizwa Sana" yaliyo kwenye tovuti ya Humanitarian Grand Challenge.. Maswali kuhusu Ombi hili la Mapendekezo ya Ufadhili ambayo hayajashughulikiwa katika sehemu ya Maswali Yanayoulizwa Sana hapo juu yanaweza

kuwasilishwa kwa barua pepe kwa info@humanitariangrandchallenge.org kabla ya Agosti 15, 2023.

**Lugha**

Maombi yanaweza kutumwa kwa Kiingereza na Kifaransa. Maombi yanayotumwa katika lugha nyingine hayatakubaliwa.

### 4.3 MUDA WA KUTUMA MAOMBI

| Shughuli | Tarehe muhimu |
|---|---|
| **Siku ya Mwisho ya** kufungua akaunti ya Fluxx **(**https://gcc.fluxx.io**)**<br>Kumbuka: Ikiwa ulituma ombi la ufadhili wa mradi hapo awali, **tayari** una akaunti. Ikiwa hukumbuki nenosiri lako, unaweza kuweka nenosiri lingine jipya na kufikia Tovuti kwa haraka. Bonyeza tu kwa Badilisha au unda nenosiri. | Agosti 15, 2023 |
| **Makataa ya Kuuliza Maswali**<br>Maswali kuhusu Ombi hili la Mapendekezo ya Ufadhili ambayo hayajashughulikiwa katika sehemu ya Maswali Yanayoulizwa Sana yanaweza kuwasilishwa kwa baruapepe kwa info@humanitariangrandchallenge.org | Agosti 15, 2023 |
| **Makataa ya Kutuma Maombi ya Ufadhili**<br>Maombi ya ufadhili lazima yawasilishwe **kabla ya** 14: 00 Saa za Mashariki Marekani Kaskazini (18: 00 GMT) | Agosti 22, 2023 |
| Kuarifiwa kuhusu hali ya maombi | Desemba 2023 |
| Mazungumzo kuhusu makubaliano ya ufadhili na kufanya ukaguzi | Desemba 2023 – Machi 2024 |
| Tarehe inayotarajiwa ya kuanza kwa miradi | Aprili 2024 |

### 4.4 MCHAKATO WA UKAGUZI

Mchakato wa ukaguzi wa mapendekezo unajumuisha Tathmini ya Ustahiki, Tathmini wa Uvumbuzi na Kamati ya Ukaguzi.

**Ukaguzi wa Ustahiki**
Grand Challenges Canada itakagua maombi ya ufadhili kwa msingi wa vigezo vya ustahiki vilivyoainishwa katika Sehemu ya 4.1. Maombi yasiyotimiza vigezo vya kustahiki yataondolewa kutoka kwa ushindani.

**Ukaguzi wa Uvumbuzi**
Maombi yatapatiwa alama kulingana na vigezo vilivyo hapa chini, kwa kutumia majibu ya maswali katika sehemu ya "Muhtasari wa Mradi" ya fomu ya kutuma maombi.

Kumbuka: Ukaguzi wa uvumbuzi hautatathmini uwezekano au ubora wa mpango wa mradi. Hii itatathminiwa katika hatua ya baadaye katika mchakato wa tathmini. Mapendekezo ambayo hayana uvumbuzi na umuhimu yataondolewa kutoka kwa ushindani katika hatua hii.

Vigezo vya Ukaguzi wa Uvumbuzi:

1. **Uvumbuzi**
   - Je, wazo lililopendekezwa linafafanuliwa wazi?
   - Je, uvumbuzi unawakilisha zaidi ya uboreshaji wa nyongeza juu ya mbinu za sasa?

2. **Ufaafu**
   - Je, suluhisho lililopendekezwa linashughulikia tatizo mahususi chini ya Humanitarian Grand Challenge, kama ilivyoelezwa katika Sehemu ya 2.1 na 2.2?
   - Je, suluhisho lililopendekezwa linasaidia watu walio katika mazingira magumu ambao ni vigumu kuwafikia na wameathiriwa na mizozo, kama ilivyoelezwa katika Sehemu ya 2.4?
   - Je, suluhisho linalopendekezwa linamilikiwa au kuongozwa na wenyeji? (Kumbuka: uvumbuzi unaomilikiwa na wenyeji utapewa upendeleo. Tazama ufafanuzi wa umiliki wa wenyeji katika sehemu ya 2.1)

**Tathmini ya Kamati ya Ukaguzi**
Kwa mapendekezo ambayo yanapita ukaguzi wa Ustahiki na Uvumbuzi, Kamati ya Ukaguzi wa kisayansi, maadili, kijamii na biashara, ikiwemo wataalam wa usaidizi wa kibinadamu na watu walioathirika na mizozo ya kibinadamu, watashauri kuhusu uhalali wa mapendekezo, kulingana na vigezo vya tathmini katika Sehemu ya 4.5.

Mapendekezo yataorodheshwa katika orodha tatu, moja kwa kila eneo linalolengwa lililoainishwa katika Sehemu ya 2.2. Kulingana na ubora wa mapendekezo yaliyopokewa, washirika wa Humanitarian Grand Challenge wana haki ya kupunguza lengo hadi moja au zaidi ya maeneo matatu ya Ufadhili wa kwanza (Nishati, Taarifa za Kuokoa Maisha; Bidhaa na Huduma za afya).

**Maamuzi ya Ufadhili**
Kulingana na matokeo ya Kamati ya Ukaguzi, Kamati ya Uendeshaji Ushirikiano wa Humanitarian Grand Challenge itatoa pendekezo la ufadhili kwa Bodi ya Wakurugenzi wa Grand Challenges Canada, ambayo itafanya maamuzi ya mwisho ya ufadhili kwa hiari yake pekee, ikijumuisha haki zake zilizohifadhiwa zilizoelezwa katika Sehemu ya 5.6. Ni miradi tu iliyokadiriwa kama inayoweza kufadhiliwa na Kamati ya Ukaguzi inaweza kupendekezwa kwa ajili ya ufadhili. Uchunguzi wa kutosha unazingatiwa kwa miradi yote iliyopendekezwa na Kamati ya Ukaguzi wa ufadhili. Kulingana na matokeo ya Kamati ya Ukaguzi au mchakato wa uchunguzi wa kweli, uboreshaji wa mpango wa mradi uliopendekezwa, muundo, kiasi, aina ya ufadhili na uangalizi unaweza kuhitajika wakati wa mazungumzo ya makubaliano ya ufadhili.

## 4.5 VIGEZO VYA UTATHMINI

**Athari**

- Je, suluhisho linalopendekezwa lina uwezo wa kuzalisha athari za kuokoa maisha au kuboresha maisha ya watu walio katika hatari ya kuathirika zaidi wanaoishi katika maeneo magumu kufikia katika mazingira yaliyoathiriwa na mizozo?

- Je, suluhisho linalopendekezwa linafaa utekelezaji mpana katika mazingira ya mizozo?
- Je, wazo lililopendekezwa linatumika kwa walio katika mazingira magumu zaidi katika maeneo yaliyoathiriwa na mizozo na lina uwezo wa kushughulikia ukosefu wa usawa?
- Je, suluhisho linalopendekezwa linazingatia kanuni za usaidizi wa kibinadamu?
- Je, suluhisho linalopendekezwa ilna uwezo wa kushawishi mabadiliko ya kiwango cha mifumo katika sekta ya usaidizi wa kibinadamu?

**Uvumbuzi Jumuishi**

- Je, uvumbuzi huo ni wa kijasiri?
- Je, wazo lililopendekezwa linaunganisha uvumbuzi wa kisayansi/teknolojia, kijamii na biashara?
- Ni kwa kiwango gani watu walioathirika na mizozo watahusika kwa ufanisi katika kutambua tatizo na suluhisho, kubuni, kupima na kutekeleza uvumbuzi uliopendekezwa?

**Mpango wa Utekelezaji wa Mradi**

- Je, mpango wa utekelezaji wa mradi umeundwa kuonyesha ushahidi wa dhana ya wazo kutekelezwa katika wakati na rasilimali zinazotolewa?
    - Uthibitisho wa dhana: ushahidi unaoweza kupimika unaotokana na mazingira yaliyodhibitiwa au madogo hivi kwamba suluhisho lililopendekezwa ni bora na/au lenye ufanisi zaidi kuliko mbinu za awali za usaidizi wa kibinadamu na kwamba uvumbuzi una uwezo wa kuendelea kukua kufikia kiwango cha upanuzi.
- Je, kuna uhusiano na sekta ya kibinafsi ambao utaongeza uwezekano wa mafanikio?
- Je, mpango wa kufuatilia na kutathmini athari unajitosheleza, ili kufikia hitimisho sahihi mwishoni mwa kipindi cha ufadhili?
- Je, ni kwa njia gani pendekezo linazingatia usawa wa kijinsia, uendelevu wa mazingira, na haki za binadamu na ujumuishaji?
- Je, ni kwa njia gani pendekezo linahakikisha uzingatiaji wa mazoea bora ya kimataifa katika sekta/shughuli iliyopendekezwa na mitazamo ya Usidhuru?
- Je, kuna ushahidi uliotolewa kuonyesha uwezekano wa mafanikio, na tathmini kali ya hatari za mradi, hatari za rushwa, hatari za kuelekeza misaada kwingine, hatari za usalama, na mikakati ya kupunguza hatari zinazohusishwa na pendekezo? (Hii inapaswa kujumuisha faragha na faragha ya data ya watu walioathirika, pale inapofaa, na kuzingatia wafanyakazi, watu walioathirika, jamii pana na wadau wengine wowote.)

**Uwezo wa Uongozi wa Kuchochea Mabadiliko**

- Je, Kiongozi wa Mradi na wanachama muhimu wa timu wana kujitolea na uwezo wa uongozi unaohitajika ili kuendeleza suluhisho kufikia kiwango cha uafikiaji na upanuzi?
- Je, Kiongozi wa Mradi aliyependekezwa na/au wanachama muhimu wa timu wamepata mafunzo yapasayo, wana uzoefu na nafasi ya kutekeleza kazi iliyopendekezwa katika muktadha wa usaidizi wa kibinadamu?

- Je, ni kwa kiwango gani Kiongozi wa Mradi na/au wanachama muhimu wameonyesha uwezo wa kushirikiana na wadau husika? (kwa mfano, watoaji huduma za usaidizi wa kibinadamu, mamlaka za mitaa, sekta ya kibinafsi)
- Je, Kiongozi wa Mradi na/au wanachama muhimu wa timu wameonyesha uwezo wa kuelewa na kukidhi mahitaji ya watu walioathirika katika muktadha husika?
- Je, ni kwa kiwango gani Kiongozi wa Mradi na/au timu wanatoka/kuhusiana na jamii ya ndani wanayolenga kutumikia? (Kumbuka: uvumbuzi unaomilikiwa na wenyeji utapewa upendeleo, tazama ufafanuzi katika sehemu ya 2.1)

**Thamani ya Juhudi**

- Je, upeo wa kazi iliyopendekezwa, uwezo wa Timu ya Mradi, na fedha zilizoombwa zinaeleweka na kujitosheleza na kuendana na ukubwa wa malengo ya pendekezo lililopendekezwa?
- Je, pendekezo hilo linawakilisha matumizi ya busara na yenye ufanisi ya rasilimali?

### 4.6 SHERIA NA MASHARTI YA FEDHA NA GHARAMA ZINAZOSTAHIKI

Gharama zinazohusiana moja kwa moja na utekelezaji wa mradi zinastahiki kulingana na Maagizo ya Gharama Zinazostahiki na Zisizostahili.

### 4.7 MASHARTI YA MALIPO

1. Malipo ya Awali: Malipo ya awali sawia na mahitaji ya matumizi ya fedha kwa gharama zinazostahiki zilizotabiriwa kwa kipindi cha kwanza yatafanywa baada ya kutia saini kwenye Mkataba. Malipo ya baadaye yatafanywa kupitia maendeleo ya kipindi cha robo mwaka kulingana na mahitaji ya matumizi ya fedha kwa Gharama Zinazostahiki. Kutakuwa na 5% ya kushikilia kwa kiasi cha pesa cha jumla ya kiwango kilichotabiriwa.

2. Maombi yote ya malipo ya awali na ripoti za kifedha zitakazowasilishwa zitatiwa saini na meneja mtendaji mwandamizi ambaye ni mhasibu aliyeidhinishwa.

3. Malipo Yaliyosalia: Malipo ya mapema hayawezi kuzidi vipindi viwili na hakuna wakati wowote kutakuwa na malipo ya awali yaliyosalia yanayoshughulikia mahitaji ya fedha ya vipindi viwili vinavyofuatana. Kwa mfano, kabla ya malipo ya awali kutolewa kwa kipindi cha tatu, malipo ya kipindi cha kwanza lazima yawajibikiwe.

4. Akaunti Tofauti ya Benki na Riba Iliyopatikana kwenye Malipo ya Mapema: Akaunti tofauti ya benki, yenye riba, itatumiwa kwa ajili ya mradi huu.

5. Malipo ya mwisho yatafanywa chini ya masharti haya:

a. Mradi umekamilika kulingana na Mkataba.
b. Grand Challenges Canada imepokea na kukubali ripoti ya mwisho.
c. Grand Challenges Canada imepokea cheti kinachosema kuwa majukumu ya kifedha kwa wafanyakazi, wanakandarasi au wauzaji wanaohusiana na mchango wa Grand Challenges Canada kwa Mradi huo yametolewa kikamilifu.

### 4.8 UKAGUZI WA FEDHA

Gharama za mradi zitakuwa chini ya ukaguzi wa kifedha na Grand Challenges Canada, hadi miaka saba (7) au hadi Machi 31, 2031 (aidha ya kipindi kilicho kirefu) kufuatia kukomeshwa kwa makubaliano ya ufadhili kati ya Grand Challenges Canada na mpokeaji wa ufadhili.

### 4.9 GHARAMA ZA KUTUMA MAOMBI

Hakuna malipo yatakayofanywa kwa gharama zilizopatikana katika maandalizi na uwasilishaji wa maombi ya ufadhili kwa nia ya kuitikia mwito wa Ombi la Mapendekezo. Gharama zinazohusiana na kuandaa na kuwasilisha maombi ya ufadhili, pamoja na gharama nyingine zozote alizopata mtumaji maombi ya ufadhili anayehusishwa na tathmini ya maombi, ni jukumu pekee la mtumaji maombi ya ufadhili.

## 5. Sera na Masharti ya jumla

### 5.1 HATI ZA UWASILISHAJI MAOMBI NA ILANI YA FARAGHA

Ili kusaidia katika tathmini na uchanganuzi wa miradi, maombi yote, hati, mawasiliano, na nyenzo zinazohusiana zinazowasilishwa kwa Grand Challenges Canada (kwa pamoja, "**Hati za Uwasilishaji Maombi**") zinaweza kushirikiwa na washirika wa ufadhili kama vile lakini sio tu Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID), Ofisi ya Mambo ya Nje ya Uingereza, Jumuiya ya Madola na Ofisi ya Maendeleo (FCDO), Wizara ya Mambo ya Nje ya Uholanzi, Idara ya Masuala ya Kimataifa ya Canada (GAC) na/au pamoja na washirika wengine, na huenda yakafichuliwa hadharani. Kwa kuwasilisha Hati zozote za Uwasilishaji Maombi ya Ufadhili kwa Grand Challenges Canada, kila mtumaji maombi kwa hivyo, anapeana ruzuku kwa Grand Challenges Canada, UK FCDO, Wizara ya Mambo ya Nje ya Uholanzi, GAC na Mfalme Wake kwa niaba ya Canada ("**Kwa Heshima Zake**"), na USAID duniani kote, leseni ya kudumu, isiyoweza kubatilishwa, isiyo ya kipekee, isiyo ya kibiashara, yenye bila malipo; ya kutumia, kuzalisha, kurekebisha, kubadilisha, kuboresha, kuendeleza, kutafsiri, kuchapisha, kusambaza, kuwasiliana na umma kwa njia ya mawasiliano ya simu na kuonyesha Hati za Uwasilishaji Maombi, kwa ujumla au kwa sehemu, kwa namna yoyote, kwenye vyombo vya habari, au teknolojia inayojulikana sasa au itakayoundwa baadaye, ikiwa ni pamoja na haki ya kuidhinisha wengine kufanya vitendo kama hivyo na haki ya kutoa leseni ndogo kwa wengine, kwa masharti sawia. Kila mtumaji ombi la ufadhili pia anaondoa haki zozote za kimaadili alizo nazo katika Hati za Uwasilishaji Maombi ya Ufadhili kwa ajili ya Grand Challenges Canada, wafadhili waliotajwa hapo juu, na kila mmoja wa wenye leseni zao ndogo, warithi, wawakilishi, kazi, wafanyakazi na

mawakala. Hii inajumuisha kushiriki mapendekezo na mashindano na tuzo nyingine za kifedha zinazoendeshwa na wasomi, sekta ya kibinafsi, mashirika ya kibinadamu na mashirika ya Umoja wa Mataifa.

Ombi litapitia ukaguzi wa nje na wataalam huru wa somo husika, washauri, na wafadhili wenza watarajiwa (matokeo yake yatakuwa ya siri), pamoja na uchanganuzi wa wafanyakazi. Tafadhali fahamu kuwa nakala ya ukaguzi wa nje kwa kila ombi lililowasilishwa itashirikiwa na wafanyakazi wa Grand Challenges Canada na inaweza kufichuliwa kwa Kamati ya Uwekezaji ya Grand Challenges Canada.

Tafadhali zingatia kwa uangalifu habari iliyojumuishwa katika Hati za Uwasilishaji Maombi. Ikiwa una wasiwasi wowote kuhusu ufichuaji wa taarifa za siri au za umiliki (pamoja na taarifa zinazohusiana na uvumbuzi), tafadhali tushauri haraka iwezekanavyo na katika tukio lolote kabla ya kufichua hati kama hizo kwa Grand Challenges Canada. Inapendekezwa uwasiliane na mwanasheria wako na uchukue hatua zozote unazoona zinafaa ili kulinda mali yako ya kiakili. Unaweza kutaka kuzingatia ikiwa maelezo kama haya ni muhimu wakati wa kutathmini uwasilishaji wa maombi na kama maelezo ya jumla zaidi, yasiyo ya siri yanaweza kutosha kama njia mbadala kwa madhumuni haya.

Grand Challenges Canada itajaribu kwa nia njema kuheshimu usiri wa maelezo ambayo yanapokelewa katika Hati za Uwasilishaji Maombi, ikiwa zina alama ya "Siri". Licha ya wewe kubainisha hati zenye maelezo yoyote kuwa "Siri", Grand Challenges Canada inahifadhi haki ya kufichua hadharani taarifa zote zilizomo katika Hati za Uwasilishaji Maombi kama inavyohitajika na sheria, na kama inavyohitajika kwa wafadhili wenza, washauri na wakaguzi wa nje (kama vile taasisi za serikali) ili kuzitathmini na namna na upeo wa uwezekano wa ufadhili, kulingana na kanuni zinazofaa na miongozo na sera zao za ndani. Grand Challenges Canada inakanusha kwa uwazi dhima yoyote na yote inayoweza kutokea kutokana na kufichua maelezo ya siri yaliyo katika Hati za Uwasilishaji Maombi ya Ufadhili.

Watumaji maombi ya ufadhili walio na maswali kuhusu yaliyomo kwenye Hati za Uwasilishaji wa Maombi ya Ufadhili wanaweza kuwasiliana nasi kwenye baruapepe info@humanitariangrandchallenge.org.

**Ilani ya Faragha**

Ili kufanya uchunguzi na ukaguzi unaostahili, na kusimamia na kufuatilia utendakazi wa makubaliano ya ufadhili, Grand Challenges Canada inaweza kukusanya taarifa za kibinafsi (kama vile majina, anwani, historia ya ajira, ukaguzi wa makosa ya jinai na ukaguzi mwingine wa kisheria pale inaporuhusiwa kisheria) kuhusu baadhi ya wakurugenzi na maofisa wa mtumaji maombi aliyefanikiwa, wafanyakazi, kiongozi/viongozi wengine wa mradi, na watu wengine wanaojishughulisha na mradi kabla na wakati wa makubaliano ya ufadhili. Baadhi ya maelezo haya ya kibinafsi hukusanywa kwa madhumuni ya kufuata mahitaji ya kisheria na sera zinazotumika ambazo zinatumika kwa Grand Challenges Canada na wafadhili wetu ili kuweza kutoa ufadhili na huduma na Grand Challenges Canada chini ya makubaliano ya ufadhili. Kukataa kutoa maelezo ambayo Grand Challenges Canada inahitaji ili kutekeleza uzingatiaji unaohitajika wa kisheria na kimkataba kunaweza kuathiri uwezo wa Grand Challenges Canada kutoa ufadhili na huduma kama hizo na kunaweza kusababisha kutoweza kuingia katika

makubaliano ya ufadhili nawe au kusitisha mapema mkataba wa ufadhili uliotiwa saini. *Sera ya Faragha* ya Grand Challenges Canada inafafanua jinsi Grand Challenges Canada inavyokusanya, kutumia, kufichua na kulinda taarifa za kibinafsi ambazo inakusanya na kupokea. Kwa kuwasilisha taarifa zozote za kibinafsi kuhusu wengine, unawakilisha na kuthibitisha kwamba umeidhinishwa kufanya hivyo. Ikiwa sheria inayotumika inakuruhusu au inakuhitaji utoe maelezo bila idhini, unawakilisha na kuthibitisha kwamba umetii sheria hiyo na kwamba inaruhusu Grand Challenges Canada kupokea na kufichua taarifa chini ya *Sera ya Faragha* bila hatua yoyote zaidi kwa upande wa Grand Challenges Canada. Unakubali kuondoa lawama na kushikilia Grand Challenges Canada kutokuwa na madhara dhidi ya ukosefu wako kushindwa kutii mahitaji yaliyowekwa hapa.

### 5.2 UDHAMINI

Kwa kutoa Hati zozote za Uwasilishaji Maombi ya Ufadhili, watumaji maombi wanawakilisha na kuidhinisha kwa Grand Challenges Canada kwamba wana haki ya kutoa taarifa iliyowasilishwa.

### 5.3 MKAKATI WA HAKI ZA UVUMBUZI NA KUSHIRIKI NA UFIKIAJI WENYE ATHARI

Grand Challenges Canada haiwezi kufadhili miradi ambayo haki msingi za uvumbuzi zinamilikiwa na mtu/taasisi nyingine, isipokuwa mtu au shirika hilo (i) litampa mtumaji maombi ya ufadhili haki za leseni za kutosha kwa uvumbuzi ili kuruhusu kuongeza kiwango katika LMIC; au (ii) kutia saini ahadi ya kutii Mkataba wa Kushiriki na Ufikiaji kwa ajili ya Mkakati Wenye Athari ya Grand Challenges Canada na Makubaliano ya Ufadhili.

Suluhisho zinazofadhiliwa na mpango huu zinajumuisha teknolojia bunifu, huduma, miundo ya biashara, maarifa na/au bidhaa za kukuza afya duniani katika LMIC. Utayarishaji na usambazaji wenye mafanikio wa suluhisho hizi ili kuhakikisha ufikiaji wa maana kwa walengwa katika LMIC unaweza kuhitaji kuhusika kwa, usaidizi wa, na/au ushirikiano na mashirika mengi, ikijumuisha sekta ya kibinafsi, serikali, na taasisi za kiakademia na/au mashirika yasiyo ya faida ya utafiti. Kwa hivyo, Grand Challenges Canada inasaidia uundaji wa ushirikiano unaofaa ambao ni muhimu ili kukidhi mahitaji haya ya dharura ya afya ya kimataifa. Watumaji maombi ya ufadhili watakaofaulu huhifadhi umiliki wa haki miliki katika uvumbuzi unaofadhiliwa, ikiwemo haki zile zinazotokana na matokeo ya miradi inayofadhiliwa. Grand Challenges Canada inalenga, hata hivyo, kuhakikisha kwamba haki zozote za uvumbuzi kama hizo zinatumiwa na kusimamiwa kwa njia inayolingana na kufikia malengo ya mpango huu. *Mkakati wa Ushiriki na Ufikiaji Wenye Athari* wa Grand Challenges Canada ("**Mkakati**") unaongoza mbinu ya shirika kuhusu mali miliki na watumaji maombi ya ufadhili wote wanahimizwa kuzingatia nia yao ya kuwasilisha maombi kwa kufuata Mkakati, ambayo ni pamoja na kuheshimu haki ya asili ya kujiamulia na kujitawala kwa Wenyeji na jamii nyinginezo ulimwenguni kote.

Madhumuni ya Mkakati huo ni kuelezea jinsi Grand Challenges Canada itafanya kazi na wavumbuzi ili: (1) kuwasaidia wavumbuzi kufikia athari kubwa iwezekanavyo kupitia uendelevu, nafuu za kifedha, na kueneza kadri inavyofaa, ufikiaji wa uvumbuzi wao kwa manufaa ya umma; na (2) kuwawezesha kushiriki kwa uwajibikaji maarifa na data *mpya* wanayozalisha, kwa namna ambayo itawezesha upanuzi na uendelevu, kushughulikia (badala ya kuendeleza) ukosefu wa

usawa na usawa wa mamlaka, na kuheshimu mahitaji mbalimbali, vipaumbele na maadili ya kujiamulia kwa wavumbuzi na jumuiya zao.

Watumaji maombi ya ufadhili waliofaulu watahitajika kujitolea kufuata Mkakati; kuunda Mpango wa Ufikiaji kwa ajili ya kufanya uvumbuzi wao kufikiwa ipasavyo na walengwa katika LMICs, kumaanisha kupatikana kwa upana na haraka kwa gharama zinazokubalika katika muktadha; na kutia saini Mkataba wa Kushiriki na Ufikiaji wa Athari na Grand Challenges Canada, kulingana na kanuni elekezi, zinazotumika kwa suluhu bunifu na matokeo ya mradi unaofadhiliwa na mpango huu.

Makubaliano ya Kushiriki na Ufikiaji wenye Athari yanaweza kutoa kwa Grand Challenges Canada leseni isiyo ya kipekee ya hakimiliki katika uvumbuzi unaoungwa mkono (ikiwa ni pamoja na mali miliki ya uanzilishi) na/au makubaliano ya usambazaji wa bidhaa, katika kila hali inaruhusu Grand Challenges Canada na waliopewa leseni ndogo za kutekeleza na kusambaza bidhaa, michakato, maarifa au suluhisho za LMICs ambapo watumaji maombi au washirika wao hawawezi kupata ufikivu wa maana.

Makubaliano ya Kushiriki na Ufikiaji wenye Athari yatawahitaji watumaji maombi wote kuingia katika baadhi au maagano yote yafuatayo (ahadi):

1. kufanya juhudi bora na kufanya kazi kwa nia njema ili kutoa ufikiaji ulioenea, wa bei nafuu na sawa kwa uvumbuzi unaofadhiliwa ili kufikia athari kubwa zaidi kwa wale wanaouhitaji zaidi;
2. kufanya juhudi bora zaidi na kufanya kazi kwa nia njema ili (i) kushiriki kwa uwazi na hadharani matokeo na mahitimisho ya mradi, yawe chanya, yasiyoegemea upande wowote, au hasi, katika kipindi cha miezi 12 ya kukamilika kwa mradi; (ii) kutoa machapisho yanayotokana na mradi yaweze kugundulika kwa uwazi mara moja na kupatikana mtandaoni chini ya sheria ya Creative Commons Attribution (CC BY) au leseni sawa; na (iii) kuweka matokeo ya data kwenye hazina husika ya ufikiaji wazi katika kipindi cha miezi 12 baada ya kukamilika kwa mradi au mara tu baada ya kuchapishwa, yoyote itayotokea mapema; na
3. kutambua Grand Challenges Canada katika machapisho yote yanayotokana na mradi.

Grand Challenges Canada na watumaji maombi ya ufadhili wanaweza kuendeleza ahadi zaidi zinazofaa kwa mradi wao maalum. Watumaji maombi ya ufadhili watahitajika kuandaa na kuwasilisha Mipango ya Ushiriki na Ufikiaji ambayo inabainisha ni lini na jinsi gani (i) wale wanaohitaji maelezo zaidi watapewa ufikiaji wa uvumbuzi unaofadhiliwa, (ii) lini ushiriki wa data utatekelezwa, na ikiwezekana (iii) lini matokeo na machapisho yatapatikana hadharani.

Kwa kiwango cha chini, 'data' inarejelea seti za data za mwisho, seti za data za kitakwimu na kimaelezo, na taarifa zinazoambatana nazo kama vile metadata, vitabu vya misimbo, kamusi za data, hojaji na itifaki.

Grand Challenges Canada inatambua thamani ya mali miliki na uchumishaji, na manufaa ya matumizi ya kwanza na endelevu ya data, lakini si matumizi ya muda mrefu au ya kipekee. Katika baadhi ya matukio, ulinzi wa mali bunifu, sheria au kanuni za uvumbuzi zinaweza kuchelewesha au kuzuia ufikiaji wa data. Katika hali ambapo uhalali wa kutosha umetolewa, Grand Challenges Canada inaweza kutoa ruzuku ya sehemu au ruzuku kamili kwa hitaji la ufikiaji wa data.

Watumaji maombi wanapaswa kutambua kwamba kushiriki kulikoelezwa hapo juu na ufikiaji kwa ajili ya ahadi za athari hutumika hata baada ya shughuli za mradi kukamilika.

### 5.4 Sera ya Maadili na Uadilifu wa Utafiti

Ni sera ya Grand Challenges Canada kwamba utafiti unaohusisha wanadamu, utafiti na wanyama na utafiti unaozingatia mahitaji ya ziada ya udhibiti lazima ufanywe kulingana na viwango vya juu zaidi vya maadili vinavyotambuliwa kimataifa. Ili kupokea ufadhili kutoka kwa Grand Challenges Canada, mwanzoni na katika kipindi chote cha mradi wa utafiti, watafiti lazima wathibitishe na kuandika kanuni za utiifu zilizo na kanuni na viwango vya maadili vilivyoainishwa hapa chini:

1. Utafiti unaohusisha watu lazima ufanywe kwa njia inayoonyesha, inayolinda, na kudumisha heshima kwa watu, inayojali ustawi wa watu binafsi, familia na jamii na haki.
2. Utafiti unaohusisha wanyama lazima ufanywe kwa njia inayohakikisha utunzaji na matibabu yao ya kiutu.
3. Juhudi fulani za utafiti, ikiwa ni pamoja na, lakini sio tu kwa utafiti na DNA inayotumia vimeng'enya, hatari za kibayolojia, na viumbe vilivyobadilishwa kinasaba, zinaweza kuongozwa na udhibiti na uangalizi ulioimarishwa.

Ingawa si lazima kwa maombi haya na kama inavyotumika kwa mradi binafsi, Grand Challenges Canada itahitaji kwamba, kwa kila eneo ambalo sehemu yoyote ya mradi inaendeshwa aidha na shirika la mtumaji maombi ya ufadhili au mpokeaji ruzuku mdogo au mwanakandarasi mdogo, uidhinishaji wote wa kisheria na vibali vya udhibiti kwa shughuli zinazofanywa vitapatikana kabla ya kuanza kwa shughuli iliyodhibitiwa. Unahitajika kukubali kuwa hakuna pesa zitakazotumika kujumuisha wanadamu katika utafiti hadi idhini muhimu za mashirika ya udhibiti na maadili zipatikane. Kwa maelezo zaidi, tafadhali angalia *Sera ya Maadili na Uadilifu wa Utafiti ya Grand Challenges Canada.*

### 5.5 Kujitolea kwa Uendelevu wa Mazingira, Usawa wa Jinsia, na Haki za Kibinadamu

Grand Challenges Canada imejitolea kuendeleza kanuni za uendelevu wa mazingira, usawa wa kijinsia na mtazamo unaozingatia haki za binadamu kama ifuatavyo:

**Uendelevu wa Mazingira:** Grand Challenges Canada inahitaji watumaji maombi ya ufadhili kujitolea kuhakikisha kuwa uvumbuzi hautakuwa na athari mbaya za kimazingira ikijumuisha, lakini sio tu, athari za muda mrefu na limbikizi. Watumaji maombi ya ufadhili watahakikisha kwamba usimamizi wa athari kwenye mazingira, ikiwa ni pamoja na uchanganuzi wowote, unafanywa kwa mujibu wa michakato ya mazingira na mahitaji ya Grand Challenges Canada na sheria na kanuni zote zinazotumika. Ikiwezekana, watumaji maombi ya ufadhili wanapaswa kujumuisha kuwa na athari chanya za kimazingira katika mradi wao wote.

**Usawa wa Kijinsia:** Grand Challenges Canada imejitolea kuendeleza kanuni za usawa wa kijinsia katika miradi ya uvumbuzi inayofadhili na kote katika shirika. Hasa, Grand Challenges Canada inaunga mkono malengo yafuatayo: (1) kuendeleza ushiriki sawa wa wanawake,

wasichana, wavulana, wanaume na wanaLGBTQI+ kama waamuzi katika kuleta maendeleo endelevu ya jamii zao; (2) kukuza utambuzi wa haki za binadamu za jinsia zote; na (3) kupunguza ukosefu wa usawa wa kijinsia katika kufikia na kudhibiti rasilimali na manufaa ya maendeleo. Inaaminika kuwa kuungana mkono usawa wa kijinsia ni lengo muhimu lenyewe, na kwamba kwa kutumia lenzi ya jinsia katika kutafuta na kusimamia uvumbuzi wa maendeleo, athari endelevu zitaimarishwa.

**Mtazamo Unaozingatia Haki za Kibinadamu:** Grand Challenges Canada imejitolea kuendeleza mtazamo unaozingatia Haki za Kibinadamu. Mtazamo huu unajumuisha kutambua kwamba ukosefu wa usawa na kutengwa huwanyima watu haki zao za kibinadamu. Mtazamo huu hasa unajumuisha uendelezaji wa kanuni za ushiriki, ujumuishaji, usawa, uwazi na uwajibikaji katika mradi wa mtumaji maombi ya ufadhili.

Kama sehemu ya makubaliano yao ya ufadhili, wavumbuzi lazima wajitolee kutii Sera za Grand Challenges Canada zinazohusiana na mada hizi zinazoingiliana.

## 5.6 HAKI ZA GRAND CHALLENGES CANADA

Ombi hili la Mapendekezo ya Ufadhili ni sehemu ya mpango wa utoaji ufadhili wa hiari, kumaanisha kwamba ufadhili wote utatolewa kwa chaguo la Grand Challenges Canada. Uwasilishaji wa maombi ya ufadhili hauundi uhusiano wa kimkataba kati ya mtumaji maombi ya ufadhili na Grand Challenges Canada.

Zaidi ya hayo, watumaji maombi ya ufadhili wote wanakubali kwamba hili linaweza kubadilika na kwamba masharti yote yanaweza kubadilika. Hasa, Grand Challenges Canada inahifadhi haki, kwa hiari yake pekee na bila arifa ya:

1. Kughairi Ombi hili la Mapendekezo ya Ufadhili wakati wowote na kwa sababu yoyote.
2. Kurekebisha na kutoa tena Ombi la Mapendekezo ya Ufadhili wakati wowote na kwa sababu yoyote ile. Ombi hili la Mapendekezo ya Ufadhili ni halali kuanzia tarehe 29 Juni, 2023 na linachukua nafasi ya Ombi lolote la awali la Mapendekezo ya Ufadhili ya aina hii. Sheria na masharti ya Ombi hili la Mapendekezo ya Ufadhili zinatumika kwa maombi yote yaliyowasilishwa kuanzia tarehe 29 Juni, 2023, kwenda mbele na zinaweza kubadilishwa na Ombi lililorekebishwa la Mapendekezo ya Ufadhili katika siku zijazo. Grand Challenges Canada inapendekeza ukague masahihisho yoyote ya Ombi la Mapendekezo ya Ufadhili kabla ya kuwasilisha hati zako za maombi.
3. Kukubali au kukataa ombi lolote lisilotii kanuni na sheria kwa sababu halikidhi vigezo vya kustahiki, halitii maagizo ya maombi na/au halitii maagizo ya gharama zinazokubalika.
4. Kutokubali ombi linalotokana na utendakazi wa mradi wa awali uliofadhiliwa na Grand Challenges Canada au mradi wake au mradi unaotokana na ufadhili mtumaji maombi alipewa kwa utafiti sawa au mradi unaokaribia kufanana na ule wa mmoja wa washirika wa Grand Challenges Canada au taasisi zinazoshirikiana.
5. Kuondoa ombi lolote katika hatua yoyote ambapo kuna dalili kwamba maombi hayo yaliidhinishwa kwa njia yoyote ile ya ulaghai wa maelezo.
6. Kukubali au kukataa ombi lolote au maombi yote, licha ya ukadiriaji wa programu kulingana na vigezo vya tathmini, kwa kutoa au bila kutoa ufafanuzi.

7. Kukubali maombi machache kuliko ilivyotarajiwa.
8. Kukubali maombi na kutoa ruzuku yenye kiasi tofauti cha ufadhili, muda tofauti na/au masharti tofauti na yaliyoelezwa hapo juu.
9. Kuthibitisha taarifa zozote zilizotolewa na watumaji maombi ya ufadhili kupitia utafiti huru au kwa kuwasiliana na wahusika wengine wanaochukuliwa na Grand Challenges Canada kuwa wa kuaminika na kutumia maelezo hayo kuelekeza uamuzi wa ufadhili wa Grand Challenges Canada.
10. Kurekebisha vigezo vya kustahiki na tathmini, ikijumuisha, lakini sio tu kwa vigezo vilivyotathminiwa katika hatua ya majaribio, wakati wowote.
11. Kutumia video au uwakilishi mwingine wa kutazamwa uliowasilishwa na watumaji maombi kwenye tovuti ya Grand Challenges Canada kwa ushiriki wa umma.
12. Kutotoa uhakiki au maoni kuhusu sababu zilizochangia ombi lichaguliwe au lisichaguliwe.
13. Kuunda tuzo za ufadhili ili kuunganisha washirika wa ufadhili wanaoweze kupatikana, ikiwemo wawekezaji katika sekta ya kibinafsi.

### 5.7 SHERIA TAWALA

Ombi hili la Mapendekezo ya Ufadhili na makubaliano yoyote yanayotokana yataongozwa na kufasiriwa kwa mujibu wa sheria zinazotumika za Canada na Mkoa wa Ontario. Kila mtumaji maombi ya ufadhili anakubali kwamba mabishano yoyote na yote, hatua au kesi zinazohusiana na Ombi hili la Mapendekezo ya Ufadhili iwe kwa tafsiri, uhalali, utendaji au vinginevyo, yatakuwa chini ya mamlaka ya mahakama za Mkoa wa Ontario pekee na kila mtumaji maombi ya ufadhili na Grand Challenges Canada wanakubali kabisa mamlaka ya mahakama za mkoa kama huo bila kubatilishwa.

### 5.8 USIMAMIZI WA HATARI, USALAMA, KUPAMBANA NA UGAIDI, KUPAMBANA NA UFISADI NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Ni lazima maombi yazingatie sheria zote husika za Canada, pamoja na sheria yoyote inayotumika ya kimataifa ya kupinga hongo na ugaidi. Mtu au shirika lolote lililotajwa kuwekewa vikwazo na Canada au Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa halitafadhiliwa. Tunaweza kuongeza maelezo kwenye orodha hii kadiri washirika zaidi wanavyojiunga na shindano.

Wavumbuzi wanapaswa kudhibiti hatari za hati zinazohusiana na miradi yao na mashirika yao.

Maombi ya miradi inayojumuisha kazi katika maeneo yasiyo salama lazima yaeleze kwa kina jinsi yatakavyodhibiti hatari za usalama zinazowakabili watu na mali. Mapendekezo yakichaguliwa kufadhiliwa, wakati wa mazungumzo, wavumbuzi watahitajika kueleza jinsi watakavyoepuka ufisadi na kuepuka uelekezaji wa ufadhili kwingine kutoka kwa madhumuni yaliyokusudiwa.

Kwa mfano, wakati wa mazungumzo wavumbuzi wataombwa kutoa maelezo ya sera na taratibu za shirika ili kushughulikia migongano ya kimaslahi na ukiukaji wa kifedha au ukiukaji mwingine, ikijumuisha nyingine, taratibu za kutosha:

- zinazohitaji shirika na wawakilishi wake kutangaza maslahi yoyote ya kibinafsi au ya kifedha katika suala lolote linalohusu shughuli zinazofadhiliwa, na kumtenga mtu huyo kutoka kwa suala linalohusika;
- kutambua hatua za kuchunguza ukiukaji; na
- mpango wa utekelezaji kwa wakati na mwafaka wa kurejesha fedha zozote ambazo zimekuwa chini ya ulaghai uliothibitishwa.

Wakati wa mazungumzo, uvumbuzi pia utahitaji kujumuisha maelezo ya sera na taratibu za shirika ili kutekeleza ipasavyo udhibiti wa ndani wa kuzuia utoaji hongo, ufisadi, ulaghai na hali zingine za matumizi mabaya ya pesa.

CREATING HOPE IN CONFLICT: A HUMANITARIAN GRAND CHALLENGE

# KIAMBATISHO CHA A: KUWASILISHA MATOKEO

**Vigezo Muhimu**
Ikiwa mradi wako utafadhiliwa, utahitajika kuripoti kuhusu idadi ya matokeo, ikijumuisha yale yaliyofupishwa hapa chini; kumbuka kuwa hii si orodha kamili, na matokeo yataamuliwa na timu ya mradi kwa kushauriana na Grand Challenges Canada.

**Matokeo ya Mwisho**
Matokeo ya mwisho ni athari za muda mrefu zinazotokana na uvumbuzi. Matokeo ya mwisho yanapaswa kuwa ya kufikiwa na kupimika ifikapo mwisho wa kipindi cha ufadhili. Matokeo ya mwisho ambayo Humanitarian Grand Challenge inazingatia ni idadi ya **maisha yaliyoboreshwa**; na idadi ya **maisha kuokolewa**.

**Matokeo ya Kati**
Matokeo ya kati ni mabadiliko ya muda wa kati yanayotokana na uvumbuzi. Matokeo haya yanapaswa kuwa ya kufikiwa na kupimika kulingana na muda na vikwazo vya rasilimali za mradi, na kuunganishwa moja kwa moja na matokeo ya mradi. Matokeo ya kati ambayo Humanitarian Grand Challenge inazingatia ni:

- Idadi ya watu walioathirika wanaotumia uvumbuzi
- Idadi ya watoa huduma wanaotumia uvumbuzi ("watoa huduma" ni watoa huduma au wafanyakazi wa misaada ya kibinadamu wanaotumia ubunifu huo kuokoa au kuboresha maisha ya watu walioathiriwa na mizozo).

**Matokeo ya Haraka**
Matokeo ya haraka ni mabadiliko ya muda mfupi yanayotokana na uvumbuzi. Matokeo haya yanapaswa kupimika na kufikiwa punde tu baada ya mradi kutekelezwa, na yahusishwe moja kwa moja na matokeo ya mradi. Mifano ya matokeo ya kati ambayo Humanitarian Grand Challenge inazingatia ni:

- Idadi ya watu walioathiriwa waliofikiwa kupitia shughuli za uhamasishaji
- Idadi ya watoa huduma waliofikiwa kupitia shughuli za uhamasishaji
- Idadi ya watoa huduma walio na mabadiliko katika maarifa au ujuzi kama matokeo ya mafunzo kuhusu uvumbuzi.

**Matokeo**
Matokeo ni bidhaa au huduma zinazozalishwa moja kwa moja, kuendelezwa au kutekelezwa kama sehemu ya ufumbuzi. Mifano ya matokeo ambayo Humanitarian Grand Challenge inazingatia ni:

- Idadi ya watoa huduma waliofunzwa kuhusu uvumbuzi
- Idadi na aina ya shughuli za uhamasishaji zilizofanywa
- Idadi ya kazi zilizoundwa kutokana na uvumbuzi.